Hakika Mwenyezi Mungu anapompenda mja humuita Jibril na husema: Hakika mimi ninampenda fulani basi mpende, anasema: Jibril humpenda

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu anapompenda mja humuita Jibril na husema: Hakika mimi ninampenda fulani basi mpende, anasema: Jibril humpenda, kisha anaita huko mbinguni na kusema: Hakika Mwenyezi Mungu anampenda fulani basi mpendeni, wanampenda wakazi wa mbinguni, anasema kisha anapewa kukubalika katika Ardhi, na anapomchukia mja humuita Jibril na kusema: Hakika mimi ninamchukia fulani basi mchukie, anasema; Basi Jibril humchukia, kisha ananadi kwa wakazi wa mbinguni; hakika Mwenyezi Mungu anamchukia fulani basi mchukieni, anasema: basi wanamchukia, kisha anawekewa kuchukiwa katika Ardhi".

[Sahihi] [Swahiih Muslim]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa Mwenyezi Mungu anapompenda mja muumini; mwenye kutii amri zake mwenye kujiepusha na makatazo yake humuita Jibril: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anampenda fulani basi mpende. Basi bwana wa Malaika, Jibril amani iwe juu yake humpenda, basi Jibril hunadi kwa Malaika walioko mbinguni. Hakika Mola wenu anampenda fulani basi nanyi mpendeni, basi humpenda wakazi wa mbinguni, kisha anapewa kukubalika katika nyoyo za waumini kwa kumpenda na kuvutiwa naye na kumridhia. Na anapomchukia Mwenyezi Mungu mja humuita Jibril: Hakika mimi ninamchukia fulani basi mchukie; Basi Jibril humchukia, kisha ananadi Jibril kwa wakazi wa mbinguni: Hakika Mola wenu Mlezi anamchukia fulani basi mchukieni; wanamchukia, kisha anawekewa kuchukiwa na kutofurahiwa ndani ya nyoyo za waumini.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/6458